

Shree Swaminarayan Vijaytetram

Shikshapatri – Swahili

Barua Ya Mafundisho

Shree Swaminarayan Temple Bhuj is grateful to all the devotees who have contributed to the translation of this Shikshapatri

Published by:
Shree Swaminarayan Temple Bhuj
Web Exclusive

With the blessings of:
Mahant Purani Swami Shree Dharmanandan Dasji



Shree Swaminarayan Temple - Bhuj
Tirth Dham, Bhuj, Kutch
370001, Gujarat, India
Tel: +91 2832 250231
Fax: +91 2832 250131
www.bhujmandir.org
info@bhujmandir.org

Mimi na sujudu moyoni mwangu kuhusu mkuu *Krishna*, ambaye upande wake wa kushoto amesimama *Radha*, kwenye kifua chake cha kulia hukaa *Lakshmi* ambaye ana furahishwa na sarakasi yake kule *Vrindavana*. (1)

Mimi, *Sahajanand*, mhudumu wa *Vrittalaya (vadtal)* naandika hili *Shikshapatri* kwa wafuasi wangu wote wanao kaa katika nchi tofauti tofauti. (2)

Utangulizi wa sehemu nne muhimu (3-6)

Kupitia sehemu hizi nne muhimu, mtakatifu *Bhagwan* hunyunyiza baraka zake kwa waalimu wawili wa kiroho aliyowakubali kama warithi wake na kwa wafuasi wake walio katika sehemu nne za kiroho.

Kwenye sehemu ya kwanza, wanajulikana kama *Naishthika Brahmacharis* (wateuwa wanaojishugulisha *Naishthika Vrata* maana yake, kiapo cha kutooa). *Mukundanand* hujulikana kuwa mwalimu katika hiki kiwango.

Sehemu ya pili, wamejumulika wale wafuasi, wanaoishi katika maisha ya kinyumbani (wanao oa) wanaojulikana kama *Grahasthas*. *Mayarama Bhatta* anatambulika kama kiongozi wa hiki kikundi.

Sehemu ya tatu, inataja wanawake walioolewa, wajane na wanawali.

Sehemu ya nne, inataja watakatifu (*Sadhus*). *Muktanand Swami* hujulikana kuwa mwalimu katika hiki kiwango

Ayodhyaprasad, mwanawe ndugu yangu *Rampratapa* na mjukuu wa *Dharmadev* babangu na *Raghuvira*, mwanawe ndugu yangu *Ichharam* na mjukuu wa *Dharmadev* babangu. (3)

Brahmachari wasio oa maishani mwao wanaoongozwa na *Mukundananda*, wanaoishi maisha ya kinyumbani kama *Mayaram Bhatta* na wafuasi wangu wengineo. (4)

Mabibi walio olewa na mabwana walio hai, wajane, wanawali wote wafuasi wangu na watakatifu wote wakiongozwa na *Muktanand Swami* wote wanafunzi wangu.

(5)

Kuambatana na maandiko matakatifu (*shashtras*) mimi mwenyewe nikimkumbuka maulana *Narayan*, nawaneemeshea wafuatao kwa utaratibu na unyenyekevu hali yao ya kidini (*swadharna*). (6)

Wafuasi wangu wote watajielemisha kwa kutilia mkazo, hili *Shikshapatri* yale yalijoandikwa kwa lengo la kuwa na utu wema kwa binadamu wote na vitu vyote vilivyo na uhai. (7)

Wanaofuata maishani mwao mwote sheria za utu wema wanajinufaisha na maisha yajayo raha tele duniani na kwenye maisha yajayo. (8)

Kwa wale, wakosao utu wema na kujifikiri kuwa huru watalia na kusaga meno maishani mwote. (9)

Hivyo basi, wafuasi wangu wote wataishi kuambatana na hizi sheria kwa utoleaji na uangalifu maishani mwote. (10)

Sheria kawaida ya wafuasi wote (11-122)

Wafuasi wangu hawataua au kudhuru kiumbe chochote chenye uhai duniani makusudi, ata kama ni wadudu wadogo kama chawa na kunguni. (11)

Wafuasi wangu wote hawataua ama kudhuru mbuzi au wanyama wengine kwa ajili ya kafara, kwa nia ya kufurahisha au kutuliza roho za mababu zao kwa sababu maandiko matakatifu yanathibitisha uhai kama kitu bora zaidi kwenye dini. (12)

Kusiwe hata mmoja atakaye kuwa mkatili dhidi ya wanadamu wengine ili kujinufaisha na mwanamke, mali au ufalme. (13)

Hamna atakaye jitoa uhai hata kwenye pahali pa kuhiji kutokana na mazingaumbwe ama kutokana na hasira ya maangaiko au kwa kutumia sumu au kwa kujinyonga au kujitupa kwenye maji. (14)

Nyama katika hali yoyote haitaliwa hata ingawa ni mabaki ya kafara. Hata mvinyo au pombe haurusiwi. (15)

Mtu anaweza kuwa mkatili dhidi ya mwenziye ama kuwa na hasira ya hali ya juu lakini hamna ruhusa kudhuru-kutumia silaha haina yote. (16)

Hakuna ruhusa ya kuchukuwa kitu chochote cha mwengine hata kama ni ya manufaa kidini, wala hata kuchukuwa kijiti ama maua na kadhalika bila ruhusa ya mwenyewe. (17)

Wafuasi wangu; wanaume au wanawake hawatashiriki ngono ya haramu. Hawatakuwa wakicheza kamari na michezo mengine kama hiyo. Tena hawatakuwa wakitumia miadarati kama bangi. (18)

Kukubali maji au chakula kilichopikwa na watu wa nje kumekataliwa na maandiko matakatifu. Wafuasi wangu hawatakubali hata kama kimetolewa kafara kwa *Bwana Krishna*. Ingawaje unaweza kukubalika kama kimetolewa kama kafara kwa *Bwana Jagannath* huko *Jagannathpuri*. (19)

Hakuna atakaye shuhudia mwenziwe uwongo hata kama ni ubinafsi ama kutumia matumizi ya lugha chafu. (20)

Ni haramu kutumia maneno ya matusi au matamshi machafu dhidi ya Mungu, wateuwa, pahali patakatifu, wanawali, maandiko matakatifu, watakatifu ama kuyasikia maneno machafu yakitamkwa na mkashifu. (21)

Mtu yeyote hatakubali chochote, ata kama ni aina tofauti ya mboga ingawa vimetolewa kama kafara (sadaka) kwenye mfano wa Mungu yule anayetolewa pombe, nyama na kadhalika kwake ya kafara ya wanyama kama mbuzi yanachinjwa kama sehemu ya kafara. (22)

Wakati wowote wafuasi wangu watakapoona misikiti za bwana *Shiva* ama mabwana wengine njiani, watasujudu kwa unyenyekevu na kuwaomba radhi. (23)

Hakuna atakaye puuza shughuli (kazi) yake kama mmoja wa ukoo, hamna ruhusa ya mwingine kuingilia shughuli tofauti za ukoo wake. Mtu hajaruhusiwa kufuata mafundisho ya waasi, yasiyo maandishi ya *Veda*. (24)

Hakuna atakayesikiliza maandishi matakatifu au hadithi za kidini kutoka kwenye kinywa cha anayeweza kufanya mtu kuasi njia za utakatifu za Mwenyezi Mungu au sheria za dini lake. (25)

Ni haramu kuongea ukweli iwapo itamsaliti mtu na wenzie. Mtu hapaswi kujishirikisha na watu wasiyo na shukrani ama kukubali rushwa kutoka kwa yeyote. **(26)**

Hamna ruhusa wa kushirikiana na wezi, watendao maovu, wadaganyifu wa kidini. **(27)**

Hakuna atakaye jihusisha na watu wadanganyifu wa kidini wanaotafuta mali, wanawake na anasa za dunia na kufanya dhambi. **(28)**

Usiyafuate mafunzo yasiyo na misingi yanayo mkashifu Mungu na sehemu yake. **(29)**

Mtu haruhusiwi kutumia maji au maziwa yasiyochungwa ama kutumia maji yasiyotakazwa kwa kuoga au kwa njia yote. **(30)**

Ni haramu kutumia dawa yenye nyama au pombe ama inayoagizwa na daktari mwenye tabia na nia isiyotambulika. **(31)**

Ni hatia kwa mtu kujisaidia haja kubwa au ndogo, ama kutema mate kwenye sehemu za wazi ambomo zimekaliwa na kutoruhusiwa hata na maandiko matakatifu. **(32)**

Mtu haruhusiwi kuingia au kutoka mahali kupitia mlango wa nyuma, na kuishi mahali bila ruhusa ya mwenyewe. **(33)**

Mme hatamsikiza mwanamke akihutubu ama akiongea maneno matakatifu ya Mungu. Hamna ruhusa mtu kujiingiza katika majadiliano na mwanamke, mtawala ama washirika wake. **(34)**

Mtu asionyeshe madharau kwa watangulizi wake, wakubwa, watu mashuhuri, wasomi na wanaojihami na salaa za kivita. **(35)**

Hakuna chochote kitachofanywa kwa haraka (bila kufikiria). Lakini mambo masafi (*dharma*) yatafanywa bila kuchelewa. Yafaa mtu kupeana hekima yake kwa wengine. Kila mtu atakuwa akijishirikisha wakati wote na watu wenye nia njema na tabia. **(36)**

Mtu asiende mkono mtupu mbele ya mtangulizi mwake, Mungu ama kwa kiongozi wake (sadaka yafaa kupelekwe kama toleo kwao). Mtu asivunje ahadi ya uaminifu

na kutojiingiza kwa hali ya kujisifu. (37)

Wafuasi wangu hawatavaa mavazi yasiyositri na kuonyesha sehemu zao za mwili. (38)

Onyesho la unyenyekevu kwa Mungu kwa njia yoyote hakuta zoezwa bila kufuatia sheria za kila sehemu ya kidini (kuabudu hakutaachwa kwa sehemu ya kidini). Kuabudu hakutaachwa kwa sababu ya wapumbvu kuingilia. (39)

Wanaume kwa wanawake wanaotembelea misikiti kila siku ama wakati wa sherehe tofauti tofauti, hawatakuwa wakichanganyana. Wanaume watakuwa wakishushughulikia sehemu yao na wanawake vile vile kwenye sehemu yao. (40)

Wafuasi wangu waliozaliwa mara ya pili watachukua (watakula) kiapo kwenye shirika la *Krishna* kutoka mwalimu wa kiroho (ninayemtambua) na kuvaa *rosary* (*kanthi*) mbili yatengenezwayo na *tulsi* kwenye shingo, na *tilak* - mistari miwili (umbo la 'U') - kwenye paji la uso, kifua na mikono. (41)

Tilak, alama takatifu (yaliyotajwa hapo mbeleni) yata tengenezwa kutokana na udongo nyeupe itwayo *Gopichandan* ama *sandal wood*. Itachanganywa na *saffron* na kadhalika nakutolea kama sadaka kwa *Krishna* kabla ya kutumika. (42)

Pamoja na hiyo mchanganyiko au na *kumkum*, *chandlo* - alama ya mviringo ('O') - kutatengenezwa katikati ya alama ('U') na utatolewa kama sadaka kwa *Radha* ama *Lakshmi* kabla ya matumizi. (43)

Sat-shudras wateuwa wa *Krishna* watafuata waliozaliwa mara ya pili kwa kuvaa *rosary* (*kanthi*) na *tilak*. Kwa heshima watafuata sheria zilizowekwa ajili yao. (44)

Shudras wengine watavaa *rosari* mbili ya *sandal wood* na kutengeneza alama ya mviringo ('O') kutumia *kumkum* kwenye vipaji vya nyuso zao. (45)

Wafuasi wangu, *Brahmins* ama wengine hawaitaji kuacha mazoezi yao ya kuvaa *vibhuti* (mistari mitatu zinazolala sawa sawa) kwenye paji la uso na *rudraksh rosary* (*kanthi*) kwenye shingo kama utamaduni. (46)

Maulana *Narayan* na Bwana *Shiva* watapewa mtazamo sawa kwa utambulizaji mmoja vile unavyotajwa kwenye *Veda* kama *Brahma*. (47)

Maandishi yetu matakatifu ya kale hupeana mwongozo kwa kipindi au wakati

mgumu wa mjira yasioweze kana kufanya sherehe za kidini na kupeana jawabu. Nyakati hizi uitwa “*Apad Dharma*”. Wafuasi wangu hawatachukila kimzaha , hata kama wakati wa majira magumu. (48)

Wafuasi wangu wote wataamka asubuhi kabla ya machweo, abudu *Bwana Krishna* kwa muda na baadaye waende msalani. (49)

Baadaye, watasugua meno zao wakiketi pahali pasafi, oga kwa kutumia maji safi, wajivalie nguo mbili safi. (50)

Wakikaa kwenye mkeka uliotandikwa kwenye sakafu safi ilyo takaswa wakiangalia mashariki ama kaskazini. Watajitawadha mara tatu kwa kutumia maji (hii ni utakazo na kutafanyiwa mwanzoni mwa kila sherehe la kidini). (51)

Wanaume watajifanya *tilak* kwenye paji la uso. Wanawake wanoishi na mabwana wao watafanya *chandlo* kwenye paji la uso kwa kutumia *kumkum* (unga nyekundu). (52)

Wajane hawatajifanyia *tilak* ama *chandlo* kwenye paji la uso wao. Waume na wanawake wote watajitolea katika maombi ya kimawazo kwa *Bwana Krishna*. (53)

Watasujudu kwa unyenyekevu mbele ya mfano au picha ya *Radha-krishna* na kuyataja maombi kwa *Krishna* mpaka wakati unawaruhusu. Ndipo waeleke kwenye shughuli zao tofauti tofauti. (54)

Wafuasi wangu walio *Atmanivedis* na watawa kama mfalme *Ambrish* watafanya shughuli za ukafara na maombi ya kimawazo. (55)

Baada ya maombi ya kimawazo, *Atmanivedis* watafanya maombi kwa mfano wa jiwe, chuma au *Shaligram* (jiwe jeusi takatifu) kwa kutumia matawi, maua na kadhalika yanayopatikana kwa urahisi. Baadaye watataja maombi ya *Krishna*. (56)

Watayataja nyimbo za kumsifu *Krishna* kadiri ya uwezo wao. Kwa wale wasioelewa *kisanskriti*, yatarudiya majina matakatifu ya *Bwana Krishna*. (57)

Baada ya haya, watamtolea chakula kwa mfano wa *Bwana Krishna* na kuyakubali yaliyotolewa kwake. Kwa hivi, wataishi maisha ya kujitolea kwa Mungu. (58)

Atmanivedis wanajulikana kama *nirguna* kwa maana shughuli zao zinakuwa *nirguna* (yasiyo na matamanio ya kidunia) vile wanavyojitoa kwa Mungu ambaye

ni *nirguna*. (59)

Hawa *Atmanivedis* hawatatumia matawi, matunda au maji kabla kuyatoa kama sadaka kwa *Bwana Krishna*. (60)

Wafuasi wangu wote wasioweza kufanya maombi kwa mfano wa *Bwana Krishna* kutokana na umri, magonjwa, au haina yote ya bahati mbaya watapea nafasi kwa wale wenye afya. (61)

Wanafunzi wangu watatoa maombi kwa yale ambayo ni mifano ya *Bwana Krishna* yaliyotawazwa kulingana na sheria za walimu wa kiroho (wafuasi/warithi wa *Dharmadev*). Kwa mifano mengine watasujudu na kunyenyekea. (62)

Wafuasi wangu wote wataenda msikitini mwa *Bwana Krishna* kila jioni kuimba na kusifu majina ya *Bwana Krishna* kwa sauti. (63)

Wataongea na kusikiza maongezi matakatifu kumhusu *Bwana Krishna* kwa ustaha na siku za sherehe, wataimba nyimbo za sifa ya kiandamana na vinubi. (64)

Wafuasi wangu wote watafuata kanuni za kila siku kuambatana na maagizo kwenye haya yaliyopita. Watajifunza maneno matakatifu yaliyoandikwa kwa *kisanskriti* ama katika lugha zao jinsi wanavyoweza kuyaelewa. (65)

Wafuasi wangu watakuwa na mtazamo wa kindani kuhusu uwezo wa mtu kabla ya kuajiriwa. Mtu atapewa kazi kulingana na uwezo na uzoefu wake. (66)

Wafuasi wangu wote watahitajika kuwajibika na hali ya watumwa wao kwa kuwapatia chakula cha kutosha, nguo na mahitaji mengine muhimu. Mshahara yatalingana na haina ya kazi na uwezo wa bwana mwajiri. (67)

Kwa kuongea na wengine, wafuasi wangu watazingatia wakati, mahali na hali ya msikilizaji kwa kutumia lugha fasaha kulingana na sherehe. (68)

Wafuasi wangu wataheshimu na kuthamini kwa unyenyekevu kwa kupeana kiketi, maji na kadhalika kwa watu wazee, waalimu, mfalme, wasiojiweza, wasomi na wahiji. (69)

Hakuna atakayekaa guu moja pajani au magoti mawili yakifungwa na chanda mbele ya mwalimu, mfalme, mfano wa Mungu na kusanyikoni. (70)

Wafuasi wangu hawatajihushisha kwenye mabishano na waalimu wa kiroho. Lakini watamheshimu huyo mwalimu kwa kumtolea chakula, fedha (pesa), nguo na kadhalika, kulingana na uwezo wao. (71)

Kwa kupokea habari ya matembezi wa mwalimu wa kiroho, wafuasi wangu watampokea kwenye mwingilio ya mji na watamsindikiza mpaka nje wa mji kwa kumtakia kila la heri. (72)

Wafuasi wangu hawatajihushisha na matendo ambayo yanahitilafiana na mafundisho matakatifu. (73)

Wafuasi wangu watafuata utu wema wa watu wakuu wa kale, wakijiepusha na matendo yao mabaya. (74)

Wafuasi wangu hawatatoa siri ya wengine kwa mtu yoyote. Watapeana heshima kuu kwa wanaohusika (kutokana na uzazi, uwezo, mila na kadhalika) bila kusawazisha watu wa kimo cha chini na wa kimo cha juu. (75)

Wafuasi wangu watajiapa kujinyima wakati wa miezi minne (kuanzia mwezi wa kumi na moja wa nusu mbala mwezi, unao malizika siku ya kumi na mbili mwangazo nusu wa *Kartik*). Na wale wasioweza kufanya hivyo wataufanya katika mwezi wa *Shravan*. (76)

Yafuatayo ni njia mufti ya utimizo na yafuatwe kila siku:

1. Kusikiliza maandishi matakatifu ya Mungu.
2. Kusoma maandishi matakatifu ya Mungu.
3. Kuimba na kusifu makuu yake Mungu.
4. Kufanya maombi katika hali ya juu.
5. Kurudia dua lake.
6. Kusoma vitabu vyake vya sifa.
7. Kuzunguka mfano wake kuelekea upande wa kulia.
8. Kusujudu kwa unyenyekevu mbele ya Mungu.

Pamoja na utimizo wa kila siku ya usafi wa kidini, wafuasi wangu, watachagua

mojawapo wa njia hizi kama sheria muhimu wakati wa *chatur-maas* na kuifuata kwa utaratibu kila siku. (77-78)

Watatimiza kufunga wakati wote wa *Ekadashi* (siku ya kumi na moja ya nusu mwezi), *Janmashtmi* (kuzaliwa kwake *Bwana Krishna*) na *Shivratri*. Watasherekea siku hizi kwa furaha kubwa sana. (79)

Kwenye siku za kufunga, hepukana kulala wakati wa mchana kwa maana kutafanya kufunga kusiwe na umuhimu jinsi ilivyo pia kutoshiriki vile vile raha za ngono katika siku hizi. (80)

Kuhusu siku za kufunga, sherehe na utamaduni za shughuli za kila siku (msikitini) kwa *Bwana Krishna*, wanafunzi wangu watafuata maagizo yaliyotibitishwa na mtakatifu *Vithalnathji* mwana wa *Vallabhacharya*, mwalimu wa wateuwa. (81-82)

Watahiji sehemu takatifu kama *Dwarika*, kufanyaa sherehe za kidini kwa jinsia ya mwongozo wa maandiko matakatofu, na kuonyesha ukarimu kwa masikini ipasavio. (83)

Wafuasi wangu wataheshimu na kusujudu Miungu mitano itwayo *Vishnu*, *Shiva*, *Ganpati*, *Parvati* na *Surya* (jua). (84)

Wakati wa mapigo yanaoletwa na mapepo chafu, wafuasi wangu watataja *Stotra* ya *Narayan Kavacha* au *Hanuman Mantra*, hawatataja majina ya Miungu ya kimo cha chini. (85)

Wakati wa *lunar au solar eclipse*, kila mmoja ataweka kando shughuli zake za kila siku mara moja, kujitawadha na kudua maombi za *Bwana Krishna* mara kwa mara. (86)

Wakati wa *Eclipse (lunar au solar)* ukiisha, wataoga wakiwa wanavaa nguo. *Grahasthas* watapea zawadi kwa maskini kulingana na uwezo wao, wengine watafanya maombi kwa Mungu. (87)

Viwango vyote nne vya kidini wata jitawadha kutokana na kuzaliwa au kufa kwa mmoja wa familia, kwa siku fulani kulingana na maandishi za matakatifu. (88)

Brahmin wateuwa wangu watakuza tabia nzuri na bora sana kwa kujizuia, kuvumilivu, kujiridhisha na mengine kama hayo. *Kshatriyas* watajitafutia utu bora wa ushupvu, ukakamavu, hukarimu na kadhalika. (89)

Kiwango cha *Vaishya* watajishughulikia ukulima, biashara, uwekezaji na

kadhalika, na *Shudras* watahudumia viwango hivi vitatu vya juu. (90)

Wazaliwa mara ya pili (*Brahmin, Kshatriyas na Vaishyas*) watahudumu ‘samskars’ kumi na sita, sherehe za kila siku na *Shradha* (sherehe za mazishi) wakati ufao kuambatana na sheria za *Grihya Sutras*, kadiri ya uwezo wao. (91)

Kama wafuasi wangu wamefanya makosa makubwa au madogo kwa nia au bila nia, watafidia hizo makosa kwa kupatana na uwezo wao. (92)

Nayachukulia muhimu na kweli maandiko matakatifu nane (*Sat-shastras*) kwa filozofia na dini.

1. *Vedas*

2. *Vyas-sutra*

3. *Shreemad Bhagwat Puran*

4. *Shree Vishnu-sahastranam kwa Mahabharat*

5. *Shree Bhagvad-gita*

6. *Vidurniti*

7. *Shree Vasudev-Mahatmya kutoka Vishnukhand ya Skand Puran*

8. *Yagnyavalkya-Smriti kwa miongoni mwa maandiko ya kidini. (93-95)*

Wafuasi wangu, wanaojitakia mema watasikiliza hizi *Sat-shastras* nane. Wazaliwa mara ya pili (*Bhramins*) watasoma, kuhubiri na kutangaza mafundisho yaliyotajwa hapo mbeleni. (96)

Baina ya mafundisho haya, wafuasi wangu watatayanisha *Yagnyavalkya-Smriti* wakisaidiwa na *Mitakshara* kama mwongozo wa kushughulikia mambo yanayo tokana na shughuli za kila siku. (97)

Sehemu ya tano na ya kumi ya *Shreemad Bhagwat Puran* yate chukuliwa kuwa hali ya juu kwa uwazi wa maelezo wa ukuu na utukufu wa *Bwana Krishna*. (98)

Msimamo wangu ni kwamba sehemu ya kumi ya *Shreemad Bhagwat Puran* kama *Bhakti Shashtra*, sehemu ya tano ya *Shreemad Bhagwat Puran* kama *Yoga Shashtra* na *Yagnyavalkya-Smriti* kama *Dharma Shashtra*. (99)

Maelezo za *Vyas-sutra (Vedanta-sutra)* na *Bhagvad-gita* zote za *Shree Ramanujacharya* yanakubalikana na mimi kama muhimu kwa filozofia na maamuzi ya kiroho. (100)

Kwenye maandiko matakatifu, sehemu zinazo tukuza *Bwana Krishna* na umuhimu wa *Dharma* (shughuli za kidini), *Bhakti* (utumizi kwake Mungu), *Vairagya* (ujinyimaji) yafaa ya zingatiwe kama sehemu muhimu zaidi. Umuhimu wa sehemu hizi ni kwamba mtu na ajitolee katika utumitumishi wake Mungu na wakati huo huo kuyashughulikia huduma za kidini pia. **(101-102)**

Dharma (dini) itajulikana kwa matendo ya mtu iliyoshuhudia na *Shruti (Veda)* na *Smritis* (kama *Manu-smriti*, *Yagnyavalkya-smiriti* na kadhalika.). *Bhakti* (utumizi kwa Mungu) utajulikana pendo lisilo na kiwango kwa *Bwana Krishna* kutokana na utambulizi wa ukuu wake. **(103)**

Vairagya (kujinyima) itajulikana kutojihushisha na malimwengu isipokuwa *Bwana Krishna*. *Gnan* (hekima) itajulikana veleuevu wa hali ya juu kuhusu *Jiva* (nafsi), *Maya* (kiumbe) na *Ishwar* (Mungu). **(104)**

Jiva hukaa kwenye roho. Yeye ni sehemu ya atomi isiyogawanyika, mtamulizi, hekima, huenea kote kwa mwili. Yeye hawezi kugawanyika, kupenyeka na kuharibika, hana mwanzo wala mwisho na kadhalika. **(105)**

Maya ni uwezo wa Mwenyezi Mungu ambayo utatu wake ni (*Satva, Rajas, na Tamas*), inayosababisha umoja wa usaikolojia kati ya *Jivatma* na mwili wake vile vile *Jivatma* na ulimwengu kupitia kwa mwili. **(106)**

Ishwara ndiye Mungu, yeye kama kiongozi huru, yu ndani mwa *Jiva*, kama vile *Jiva* yumo mwilini, ambaye ni mtawala mkuu na yule anayemzawadia *Jiva*, matunda ya matendo yao (karma mazuri au mabaya). **(107)**

Huyo Maulana ni *Shree Krishna*. Anaitwa kama *Parbrahma, Puroshottam*. Ni chanzo cha kila kiumbe. Yeye ni Mungu wetu mpendwa. Yeye ndiye kivutio cha usujudu na maombu yetu. **(108)**

Atajulikana kama *Radhkrishna* akiwa pamoja na *Radha*. Atajulikana kama *Lakshmi-Narayan* akiwa pamoja na *Rukmani* au *Lakshmi*. **(109)**

Ataitwa *Narnarayan* akiwa pamoja na *Arjun*. (Pia kama Rama-Krishna akiwa pamoja na *Balarama*.) **(110)**

Wakati mwingine *Radha* na wengine abao wametajwa hapo kitambo, waonekane kando mwa *Shree Krishna* na wakati mwingine wajumlishwa ndani mwake, kutokana na mapenzi ya hali ya juu. Hapo ata-tambuliwa kuwa mmoja. **(111)**

Kwa hivyo, kusiwe na yeyote atakaye eliwa vibaya ati *Krishna* ni tofauti na *Narayan*, au *Rama-Krishna*, au *Radha-Krishna*. Yeye ujitokeza kwa hiari yake akiwa na mikono miwili, wakati mwingine mikono minne au zaidi. **(112)**

Watu wote ulimwenguni watajitoa wakfu kwa *Bwana Krishna* pekee. Yafaa iziingatiwe kwamba hamna njia yoyote ya wokovu ila kujiweka wakfu kwake Mungu pekee. (113)

Lengo kuu na muhimu kuwa na utu wema ni kutafuta uhusiano ulio takatifu kwake maulema *Krishna* na kuwa na shirika safi la wafwasi wake wazuri. Ikiwa lengo hili halitatimizwa, hata wasomi watapata majuto yao. (114)

Wateuwa wangu watamsujudu maulana *Krishna* na wahusika wake na sanamu ya picha yake. Hawata sujudu kwa roho *Jiva* yeyote ingawa wameweza kuwa watakatifu au wafuasi wakuu ama mwonaji wa *Brahma*. (115)

Kupitia *Yoga*, wafuasi wangu watatofautisha roho na sehemu tatu tofauti za mwili (*Sthula, Sukshma na Karana shareers*) na afurahie utofauti wake wakipekee. Ndiposa watatambua kuwa ubinafsi ni *Rupam* wa *Brahman* (umbo au mwili wa *Brahma*). Kasha wataweka mawazo yao ndani ya *Bhakti Yoga* (hayo mawazo yatabadilika kuwa kama *Bhakti* kwake *Maulana Krishna* – roho usiofilisika. Wote watajizoesha kufanya hivi ingawa ni ngumu). (116)

Wote watasikiliza kwa heshima sehemu ya kumi ya *Shreemad Bhagavata* kila siku ama mara moja ingawaje kwa mwaka. Wasomi watasoma na kutoa hatuba kila siku au mara moja kwa mwaka. (117)

Kulingana na uwezo wao, wateuwa watapanga kwa ajili ya mazungumzo ya sehemu ya kumi ya *Shreemad Bhagwat*, au *Vishnu-shahasra Nama* au maandiko matakatifu (uliotajwa hapo mbeleni), kupitia kwa watakatifu *Brahmins*, katika pahali patakatifu. Hivi, kutaleta mazao yanayotarajiwa. (118)

Watafuata mwongozo huu wa tabia ile wajilinde na wengine kutokana na maradhi au ugumu wowote utakao tokea kwa makosa ya binadamu au hali ya kawaida. Wasiwe watu wasiojali. (119)

Watatilia maanani, mahali, wakati, sehemu ya umbo, umri, hali yao ya kifedha na uwezo wanapo tekeleza jukumu yao ya kidini na tabia za kidini. (120)

Wafuasi wangu wote wataelewa kwamba shule langu la *Vedanta* ni *Vishishtadwait* ya *Bwana Ramajuna* na pahali pangu pa upendo ni *Golok Dham* na *Mukti*, mtu atatumainia kupata mwili mtakatifu katika *Dhaama* kama ule wa *Brahma* na kutoa hudumu kwa maulana mtakatifu *Krishna*. (121)

Umuhimu wa sheria za kidini vile ulivyoenezwa ni sawa kwa wafuasi wangu wote wanaume na wanawake. Sasa nitaeleza umuhimu wa sheria za vikundi tofauti. (122)

Sheria muhimu ya waalimu wa kiroho (Acharya) (123-132)

Vijana wawili (*Shree Ayodhyaprasadji Maharaj* na *Shree Raghuvirji Maharaj*) wa ndugu makubwa na mdogo mtawaliao hawatapeana *mantras* ama kipo kwa wanawake wasio na ukoo wakaribu katika jamii moja nao. (123)

Waalimu wa kiroho wazoa wangu walio wateuwa na viongozi hawatawaguza au kuwaongelesha wanawake kama hao (waliotajwa hapo mbeleni). Hawatakuwa wakali kwa yeyote wala hawatawekea mtu yeyote mali au chochote kile kwa ulinzi wao. (124)

Hawatajiweka kama wadhuini kwa mtu yeyote kwenye shughuli za kimaisha au kisheria. Wakati wa masumbuko kifedha wataishi kutokana na utoleaji na hawatakuwa wadeni. (125)

Hawatauza nafaka ambazo wametolewa na wafuasi wao, lakini wanaweza badilishana kwa maana hivyo sio sawa na kuuza. (126)

Watamsujudu bwana makatifu *Ganesh* siku ya nne, mwezi wa *Bhadrapada* na kwa mtakatifu *Hanumanji* wakati wa siku ya kumi na nne wa mwezi *Ashwin* kila mwaka. (127)

Nimewapa ukuu wote wawili kwa nia ya kuilinda na kuhifadhi dini yetu. Watawaweka wakfu wale wanafunzi walio na haja kamili ya wakovu (*Mukti*). (128)

Watadumisha nidhamu miongoni mwa wanafunzi na kuona kuwa wafuasi wanafuata sheria vilivyo na kutenda kazi zao za kidini. Wataheshimu watakatifu na kuyasoma *Vedas* na *Shashtras* kwa unyenyekevu. (129)

Watatoa na kwendeleza huduma jusi ilivyotajwa katika maandiko matakatifu-kwa miungu kama vile *Lakshmi-Narayan* na wengine nilio waweka mimi hadhifu kwenye misikiti kubwa na ndogo. (130)

Akujaye msikitini kutafuta chakula atashughulikwa kwa heshima kwa kupewa chakula kwa kadiri ya uweza wao. (131)

Wataanzisha “*Pathashalas*” (chuo cha elimu) na kuwateuwa *Brahman* wasomi kuyashughulikia, kutangaza *Vedas* na *Shastras* yanayoitwa *Sad-vidya*. Hiki ni kitendo cha hali ya juu. (132)

Sheria muhimu ya mke wa Acharya (mwalimu mkuu) (133-134)

Mkewe mwalimu mkuu wa kiroho, kwa ruhusu ya mumewe atapeana *mantra* (maombi maalum) ya *Maulana Krishna* kwa wanawake pekee. (133)

Hawata guza, wala kuongelesha au kuonyesha uso wake kwa mwanaume asiye wa ukoo wake wa karibu. (134)

Sheria muhimu ya wachumba (Grahasthas) (135-156)

Wachumba (*Grahasthas*) walio wafuasi wangu hawatamguza mwanamke mjane asiye wa ukoo wa karibu nao. (135)

Hawatakaa mahali pa siri, na mama, dada au binti, walio na umri mdogo isipokuwa wakati wa dhanera na hawatawapeana wake zao kama matoleo kwa mtu yeyote. (136)

Hawatakuwa na uhusiano wowote na mwanamke mwenye shuguli na mtawala kwa madhumuni yanayojulikana ama yasiojulikana. (137)

Watawapokea wageni watakao kuja nyumbani mwao kwa kuwalisha na kadhalika kwa ubora na ustarabu. Watapatia dhahibu kwa Miungu na *Shradha* kwa wazazi na mababu waliofarika jinsi ilivyo katika maandishi matakariifu. (138)

Kwa vyovyote vile, wafuasi wangu watawashugulikia mama, baba, wakuu na mgonjwa kwa kuwatunza vyema wakiwa wangali hai. (139)

Kwa vyovyote vile, watajishughulisha na kazi zinazowafaa kutokana na *Varna* na *Ashram*. Walio wakulima hawatafunga uzazi wa ng'ombe ndume. (140)

Wataweka pesa na nafaka wakati wa mwaka kwa shughuli za baadaye, kulingana na uwezo wao. Wanaofuga ng'ombe wataweka chakula cha ng'ombe cha kutosha. (141)

Wachumba waweza kufuga ng'ombe iwapo wana uwezo wa kuwatunza vyema, la sivyo hawaruhusiwi. (142)

Bila maandishi yalioitiwa sahihi na mashahidi, wafuasi wangu hawataingilia shughuli za biashara, kama ununuzi wa mali, kukopesha ama kukopa pesa kwa mtu yeyote, hata kama ni kijana wake au rafiki. (143)

Wanapojiingiza kwenye maelewano ya ndoa, wasiegeme makubaliano ya maneno yao pekee. Wataandikishana barua na kuwekania sahihi na mashahidi wao. (144)

Watatumia pesa kulingana na hali ya mapato yao. Watakuwa wakitilia mkazo kwamba utumizi mbaya utawaletea fedheha. (145)

Mara wanapomaliza kusanya mapato ya kila siku na matumizi yao wataweka rekodi safi ili kuwa na mfuatilio bora. (146)

Watamtolea *Maulana Krishna* fungu la kumi ya mapato yao. Wachumba (*Grahasthas*) walio na mapato ya kadiri watatoa moja kwa ishirini wa mapato yao. (147)

Watakuwa wakihudhuria na kusherekea sherehe za kidini kama kufunga wakati wa *Ekadashi* na mengine kama hayo, jinsi vilivyo kwenye maandishi ya kidini kwa uwezo wao. Hayo sherehe za kidini yatatimiza mahitaji yao. (148)

Wakati wa mwezi *Shravan*, watashughulika kulingana na maombi za kusujudu kwa bwana *Mahadev (Shiva)* kwa kumtolea matawi ya *bilva* na maua. (149)

Hawatakopesha pesa kutoka kwa mwalimu wa kiroho (*Acharya*), kutoka msikitini mwa *Bwana Mtakatifu Krishna*, ama kukopesha vyombo, shanga au nguo ama vitu vya matunzi ya kibinafsi. (150)

Wakati wa kuhiji kwa ajili ya kuabudu *Bwana Krishna*, ama mtakatifu au mwanzishi, hawata kubali chakula kinacholetewa na wengine wanaoelekea sehemu hizo za kuhiji, maana matendo kama haya yanatupokonya matunda ya utu wetu kama usafi na ubora wa kuhiji. (151)

Atamlipa mfanyazi kazi ajara kulingana na maelewana, hutamlipisha duni. Hatakuwa na shughuli na waasi. (152)

Wakati wa kiangazi, njaa na tumizi mabaya na maadui na watawala yanayoweza kuleta hasara, upotevu wa mali ama maisha, wafuasi wangu watahudhulika kivanja cha kuhama nchi yao na kutafuta utulivu mahali mwingine. (153-154)

Wale wachumba (*Grahasthas*) wanaouwezo wa kijuu watatoa sadaka kwa 'Yagnas' isiyo na doa ya kuuwa mnyama. Watalisha watawa (*Brahmins*) na wahiji wanaokaa pahali pa kuhiji, na siku mtakatifu. (155)

Watapanga sherehe wakati mkuu msikitini na kupeana sadaka kwa watawa wahitaji. (156)

Sheria muhimu ya watawala (157-158)

Wale watawala waliowafuasi wangu watawlinda waliochini wao vile wanavyo fanya kwa watoto wao kufuatana na sheria za kidini. Wataweka msingi utuwala wa kidini ulimwenguni. (157)

Watawala watahitaji ulimu wa juu: 1) sehemu saba za utawala, 2) njia nne za upotovu, 3) njia sita za kidiplomasia. Watausoma na kuelewa kwa umakini hali ya wapepelezi wanaotambuliwa katika sehemu tofauti tofauti za utawala. Watachagua watu wanaonui kwa waziri na watakuwa na uwezo wa kutambua wanaohitaji kuhukuniwa na wale hawajihitaji kuhuniwa. (158)

Sheria muhimu ya wanawake waliyo-olewa (159-162)

Mabibi wale mabwana wao wako hai watawahudumia mabwana wao jinsi ya kumhudu mia mwenyezi Mungu. Hawata tumia maneno makali kwa mabwana wao, hata kama yeye ni kipofu, mgonjwa, kutokuwa na uwezo wa kuzaa au maskini. (159)

Hata jihushisha kwandani au kijujuu na mme yoyote isipokuwa bwana wake hata kama yeye ni wa utu mema. (160)

Mwanamke bibi hatatenda kwa jinsi ileisiofunika sehemu ya uzazi, mapaja na matiti na ileinakaribisha wanaume wengine. Hatawa tazama kwa matamairo wengine na kutojhusisha mwanamke haramu. (161)

Wakati mabwana wao hawako nyumbani, wanawake mabibi hawatavaa nguo ya hali ushanga au uremba. Hawatakaa kwenye nyumba ya wengine wala kusherekea pamoja na wanawake wengine. (162)

Sheria muhimu ya wajane (163-172)

Wajane watamhudumia Mwenyezi Mungu kwa niaba ya mabwana wao na kukaa na baba wao, ndugu au vijana. Hawatasimamia kibinafsi. (163)

Hawatanguza mme wowote asiye na ulusiano wa karibu nao. Wajane wa miaka nchache hawatawaongelesha vijana bila mahitaji maalum. (164)

Kumguza mtoto mdogo haina mahadhara kama kumguza mnyama. Kumguza au kumwongelesha mzee haina mahadhara, ikiwa haiwezi ikaepukika. (165)

Kujifundisha mambo yenye manufaa kutoka kwa mme yule asiyekaribu nawe yana faa kuepushwa. Wajane watajitawala kimwili na kwa njia za kufunga na unyimaji. (166)

Rasilimali yanayowekwa na wajane hayata tumika kwa njia ya *filanthropia*. Atapeana iwapo anazo za zaidi. (167)

Watakula mara moja kwa siku na kulala sakufuni. Hawata watazama wanyama wanapo jamiana kingoni. (168)

Hawatajivalia kama waliyolewa ama wanawake watawa, au mwamamke ruhribifu. Hawatajivalia nguo yasiyo ya heshima. (169)

Hawatakuwa na urafiki ama kuwaguza wanawake wanaojishullosha na uwavimbia (*abortion*) wala hawataongea au kuwasikiliza wanaume wenye maongezi machafu wa wanaume. (170)

Isipokuwa katika hali ya udharura, mjane yule wa miaka michache hatakaa pamoja na kijana mdogo wakiwa sehemu pasipo na watu, iwayo wa ukoo wakiwepo karibu. (171)

Wajane hawatacheza '*Holi*' na kutojihushisha na kuvaa ushanga au nguo nyepesi yanayotengenezwa kwa kutumia hariri au nyuzi za dhahabu. (172)

Sheria muhimu ya wanawake wote (173-174)

Wanawake hawataoga bila nguo na hawataficha wakati wao wa hedhi. (173)

Wakati wa hedhi, ni haramu kumguza binadamu, nguo na vyombo vingine mpaka siku tatu. Wako huru kufanya hivyo siku ya nne baada ya kuoga. (174)

Sheria muhimu ya Naishthika Brahmacharis (175-187)

Naishthika Brahmacharis ambao ni wafuasi wangu hawataguzi, kuongea, au kutazama wanawake ovyo ovyo. (175)

Hawataongea kuhusu wanawake na hawatajihusisha na sheria za kuoga, *Sandhya Vandan* na kadhalika kwenye sehemu zinazotembelewa na wanawake. (176)

Hawataguzi ama kutazama michoro au picha (sanamu) za wanawake ikiwa imetengenezwa kutumia mbao au chuma, ijapokuwa sanamu ya Miungu. (177)

Hawatajichongea au kuchora picha za wanawake wala kuguzi nguo ambazo zimevaliwa na wanawake. Hawata kutazama wanyama kwa nia ya kingono. (178)

Hawatamtazama au kumguzi mwanamume anayejifanya kama mwanamke wala imba nyimbo za sifu wa Mungu mbele ya wanawake. (179)

Hawataheshimu sheria anayokeshifu kiapo chao cha kutoa hata kama iatolewa na walimu wa kiroho (*guru*). Wataishi maisha ya muitoshelesha kihisia na unyenyekevu. (180)

Mwanamke wowote akijaribu kuwakaribia, watamkataza kwa kuongea na yeye au kuonyesha dharau kwake. (181)

Wakijua ya kwamba maisha yao au maisha ya huyo mwanamke yako hatarini, watam-msuru au kujiusuru kwa kumwongelelesha ama kumguzi. (182)

Hawatajisugua mwili kwa mafuta wala kuweka vifaa vya kivita, wala kujivaa kipumbavu. Watazua husia yao ya kunusha. (183)

Hawataingia nyumbani mwa wanawake. Wataenda kwa watawa na kushugulikiwa na wanauwe. (184)

Watajifunza *Veda-Shastra* na watawahudumia *Guru* wao. Watajipusha na wale wanaume wenye hisia mbofu wanaojitafutua husiano tu na wanawake. (185)

Hakuna hata mmoja, *Brahmin* kwa kuzaliwa, atakunyua maji kutoka kwa mkopa wa kubebea maji au kutumia vitu kama vitunguu saumu na vinginevyo kama hivyo. (186)

Hawatakula chakula kabla ya kutimiza baadhi ya utendaji kazi wanaowajibika kutenda kidini; maisha ya kawaida kama kuoga, kufanya *Sandhya Vandan*, kurudia *Gayatri mantra*, kufanya *Vishnu pooja* na *Vaishvadeva Yagna*. (187)

Sheria muhimu ya watakatifu (Sadhus) (188-196)

Kama *Naishtika Brahmacharis*, *Sadhus* watajiepisha na ukaribiano na wanawake, na wanaopenda wanawake. Watatenga adui wao wa kindani kama hasira, choyo, kiburi na kadhalika. (188)

Watakuwa na uwezo wa kujimudu kihisia hali yao ya kuonja. Hawatajipatia au kujiwekea pesa ama kuruhusu wengine wafanye hivyo kwa niaba yao. (189)

Hawatawekea wengine mali yao au kukubali chochote kama dhamana. Watakuwa na uvumilivu wa hali ya juu. Hamna ruhusa ya kuwakaribisha wanamke pahali pao pa kukaa. (190)

Isipokuwa wakati wa dharura, hawataenda nje wakati wa usiku pekee yao. Hamna ruhusa kutembea mmoja wakati wowote. (191)

Hawaruhusiwi kuvaa nguo ghali, yaliyo na maua maridadi yaliyo na mshono ya haina tafauti, hatakama amepewa kama zawadi. (192)

Ni haramu kuwatembelea makazi ya wachumba (*grahastas*) ijapokuwa wakati wa maombi au shudhuli za kidini. Wao (hata kwenye makazi yao wenyewe) watatumia wakati wao kwa dini ya Mwenyezi Mungu baadala ya kupoteza wakati wao. (193)

Watakubali chakula kutoka kwenye nyumba ya mpokezi mwanamume, mahali hutakuwa na uwezo wa kukutana na wanawake. Ikiwa hautawezekana, basi watapewa fursa na mpokezi wakujiandalia mamkuli. (194-195)

Maishani mwao kulingana na hali ya kimaisha watafuata utu mema wa *Jada Bharat*, mwana wa *Rushabhadev*. (196)

Sheria muhimu ya Naishthika Brahmacharis na Sadhus (197-202)

Naishthika Brahmacharis na *Sadhus* watajiepusha kwa vyovyote kutafuna mbaki au tombako na kutumwa mihadarti kama bhangi. (197)

Wote wawili hawata kubali chakula (kwenye nyumba ya wachumba) wakati wa *Sankaars* kumi na sita, mifano kama sherehe za watu yanayo shughulikiwa siku za kumi na moja, na kumi na mbili. (198)

Hawatajilalisha wakati wa mchana isipokuwa wakiwa wagonjwa. Hawataongea au sikiliza maneno matupu. (199)

Hawatajilalisha kitandani isipokuwa ni wagonjwa. Watakuwa na tabia nzuri bila kujifanya mbele ya watakatifu. (200)

Watakapo shambuliwa na maneno makali au kupigwa na wasio wazuri, hawatalipiza kisasi. Watawasamehe na kuwaombea mema. (201)

Hawatajihushisha na shughuli za watumizi ama mpelezi. Hawatakuwa na udanganyifu wa mwenyewe kama mwili. Hawatafungiwa na familia zao. (202)

Mwisho (203-212)

Hivyo, sheria za utu kwa wafuasi wangu wote zime andikwa na mimi kwa mukhtasari (ufupi). Kwa kinaganaga, mmoja atapitia maandishi matakatifu yaliyokubalikwa na kikundi yetu. (203)

Shikshapatri (waraka wa sheri) umeandikwa na mimi, baada ya kufuatilia kwa ustadi maandiko matakatifu. Hii *Shikshapatri*; utawakamilishia matamano ya wafuasi wangu. (204)

Kwa hivyo, wafusi wangu watafuata kwa makini hii *Shikshapatri* na kuishi jinsi vilivyo, lakini hawatatenda wapendavyo wenyewe. (205)

Ni wazi kwamba wale waume na wanawake wanaofuata mwelekeo huu watapata *Dharma* (utu), *Artha* (mali), *Kama* (raha) na *Moksha* (wokovu). (206)

Wafuasi wangu wote wataelewa ya kwamba wasiofuata *Shikshapatri* jinsi ilivyo, watachukuliwa kama waasi wa kukundi chetu. (207)

Wafuasi wangu, watajitahidi kukisoma hiki kitabu kila siku. Wasio na uwezo wa kusoma watakisikiliza kwa makini. (208)

Iwapo hamna mtu wa kusoma (masomaji) na kuwahadithia, watakiabudu hii kitabu kwa ustaha, kwa kuichukulia *Shikshapatri* kuwa mfano wangu mimi mwenyewe. (209)

Hii *Shikshapatri* kutapewa wale wenye utu bora wala sio kwa wale wasio na utu njema. (210)

Hii *Shikshapatri* wa baraka njema uliandikwa siku ya kwanza wakati wa kusherekea *vasant utsava (Vasant Panchmi)* mwaka wa 1882 wa wakati wa *vikram (A.D 1826)*. (211)

Maulana Krishna huondoa maguma yote kwa wafuasi wake. Huwalinda na kuwaimarisha kidini (*Dharma*) na utawa (*Bhakti*), kwa wafuasi wake. Yeye hupeana raha ya hali ya juu wanayohitaji. Nawaombea wote baraka, heri mjema na fanake kutoka kwake kwetu sisi wote. (212)

Hapo ndipo kikimo cha *Shikshapatri* iliyoandikwa na *Bwana Mtakatifu Swaminarayan*.

UTUKUFU KWA MTAKATIFU SWAMINARAYAN

--Jay Shree Swaminarayan--